sustainable sanitation alliance

# Mwelekeo kwa suluhu la usafi himiliki

Version 1.2 (February 2008)

Kiswahili translation (July 2009)

## Utangulizi

Huku ikizingatiwa kuwa watu bilioni 2.6 duniani hawana aina yoyote ya usafi ulioimarishwa, haja ya hatua mwafaka kuchukuliwa katika uwanja wa usafi ni bayana. Uhitaji huu unalazimu ikizingatiwa kuwa watu millioni 2.2 hufariki kila mwaka (wengi wao wakiwa watoto walio na umri wa chini ya miaka mitano). Vifo hivi huzuliwa na magonjwa yanayohusiana na usafi na hali mbaya za usafi.

Umoja wa Mataifa ulizua safu ya mfululizo wa Malengo ya Milenia (MDGs) katika mikutano miwili muhimu: mkutano wa milenia mjini New York mwaka wa 2000 na ule wa kimataifa kuhusu maendeleo himiliki. Lengo la kuwa na malengo ya milenia lilikuwa ni kuondoa umasikini na kudumisha maendeleo himiliki. Lengo mahususi lililowekwa kwa utoaji wa maji na huduma za usafi lilikuwa kupunguza idadi ya watu ambao hawana maji safi ya kunywa na huduma za kimsingi za usafi kwa asilimia 50 (50%) ifikapo mwaka wa 2015. Kulingana na ushahidi wa programmu ya pamoja ya usimamizi pamoja na ripoti ya maendeleo ya jamii kutoka shirika la UNDP, hatua za kuafikia lengo la milenia kuhusu usafi ni za pole pole sana. Aidha, imebainika kuwa kuna tofauti kubwa sana kati ya yaliyokusudiwa na uhalisia wa sasa kuhusu usafi hususan katika Afrika ya Sub-Sahara na sehemu za Asia. Sababu za hali kuwa hivi ni nyingi. Miongoni mwazo ni ukweli kuwa usafi/ huduma za usafi hazipewi kipaumbele na wanasiasa, serikali na raia. Aidha, Ridhaa ya kisiasa haijakuwepo swala la usafi linapoangaziwa na kuzungumziwa katika ajenda za ukuaji na maendeleo. Hali hii imeufanya usafi na utoaji wa huduma za usafi kufichika katika kivuli cha miradi ya utoaji na usambazaji wa maji.

Uamuzi wa Umoja wa Mataifa wa kuutangaza mwaka wa 2008 kuwa Mwaka wa Kimataifa wa Usafi – (***International Year of Sanitation***), ulizua ari miongoni mwa mashirika tendi katika uwanja wa usafi kuunda jopo kazi kuunga mkono madhumuni ya Mwaka wa Kimataifa wa Usafi. Januari 2007, mkutano wa kwanza ulifanyika na washiriki kutoka mashirika mbali mbali wakatoa ahadi zao. Katika mkutano huu mswada wa kwanza wa pamoja wa namna ya kuanzisha na kukuza usafi himiliki uliandikwa. Mnamo Aprili 2007 mkutano wa pili uliandaliwa ambapo lengo na madhumuni ya mtandao huu wa ustadi wa kimataifa yalibainishwa waziwazi. Aidha, mswada ule wa kwanza uliangaliwa upya na kurekebishwa. Ili kufungamana na uvumbuzi unaotarajiwa na kuwa na kitambulisho sawa kwa



minajili ya shughuli zilizo/zitakazopangwa, kikundi hiki kiliunda na kuanzisha Muungano wa Mashirika Tekelezi ya Usafi Himiliki- *Sustainable Sanitation Alliance* (**SuSanA)**.

## Usafi himiliki ni nini?

Lengo kuu la mfumo wowote wa usafi ni kulinda na kujenga afya ya mwanadamu kwa kukimu mazingira safi na kuvunja mbembeo (cycles) za maradhi. Ili mfumo wa usafi uwe wa kuhimilika, ni sharti ujitegemee kiuchumi/kifedha, ukubalike na wanajamii na uwe unaofaa kiteknolojia na kitaasisi. Bali na hayo, ni lazima ulinde mazingira na malighafi. Katika kurekebisha/ kuboresha au kusanifu/kunaksi (design) mfumo mpya wa usafi, vigezo vifuatavyo vya uhimilikifu havina budi kuzingatiwa:

(1) **Afya na Usafi**: Dhana hizi huhusika na hatari inayotokana na viini ambavyo huathiri afya ya umma katika vituo vyote vya mfumo wa usafi kuanzia chooni, ukusanyaji na usafishaji wa uchafu unaotoka chooni hadi kwa urudufu (re-use) au utupaji (disposal). Dhana hizi pia hushirikisha usafi, lishe na uboreshaji wa riziki unaoafikiwa kwa kutumia mfumo fulani wa usafi. Athari zinazotokana na kutupa uchafu huu kwenye mito huzingatiwa katika kigezo hiki.






(2) **Mazingira na malighafi:** Yanayoshughulikiwa hapa ni pamoja na kawi inayohitajika, maji na aina nyingine za malighafi katika uundaji, utekelezi na udumishaji wa mfumo husika. Aidha kuna kuzingatia uwezekano wa kuwepo uvundo kutokana na matumizi. Bali na hayo, kiwango cha kurudufu, utumizi tena na athari zake (K.v. utumizi wa pili wa majitaka, kurejesha virutubishi kwa kilimo). Pia swala la kulinda na kuzuia malighafi k.m kupitia kuzalishwa kwa kawi k.v bayogesi

(3) **Teknolojia na utekelezi:** Dhana hizi hushirikisha utendaji na urahisi ambao kwao mfumo mzima (kuanzia ukusanyaji, usafirishaji usafishaji hadi urudufu (re-use) na/ au utupaji) utatengenezwa, kutekelezwa na kusimamiwa na jamii na/ au wanateknolojia wa utoaji huduma kwa umma. Bali na hayo, uwezo wa mfumo huo, wepesi wa kuathiriwa kwake na ukosefu wa umeme, uhaba na/ au ukosefu wa maji, mafuriko n.k. na wepesi wake wa kubadilika kutegemea misingi yake ya kiteknolojia kwa miundo msingi iliopo, idadi ya watu na maendeleo ya kijamii ni dhana muhimu zinazofaa kuzingatiwa.

(4) **Maswala ya kifedha na kiuchumi:** Maswala haya huhusiana na uwezo wa kaya na jamii kulipia huduma za usafi pamoja na utengenezaji, utekelezi, udumishaji na uwekezaji katika mfumo wa usafi. Bali na utathmini wa gharama, manufaa ya moja kwa moja kama vile kutoka kwa bidhaa zitokanazo na urudufu (vikolezo vya uimarishaji wa udongo (soil conditioner), mbolea, kawi na maji yaliyoongolewa) na gharama za nje na manufaa sharti yazingatiwe. Gharama hizi za nje ni k.v. uchafuzi wa mazingira na hatari za kiafya. Manufaa yaweza kuwa ongezeko katika uzalishaji wa chakula, nafasi za kazi, afya nzuri na kupunguka kwa hatari za kimazingira.

(5) **Vipengele vya kijamii, kitamaduni na taasisi**: Katika kitengo hiki, ni muhimu kuchunguza na kutathmini kukubalika kwa mfumo wowote ule kijamii na kitamaduni. Aidha ufaafu, mtazamo wa wanajamii kwa mfumo husika, dhana za kiuana na athari za mfumo husika kwa utu wa wanadamu ni maswala muhimu. Zaidi ya hayo, ni sharti kuzingatia mchango wa mfumo wa usafi katika kuhakikisha uwepo wa chakula cha kutosha, kukubalika katika sheria na katika taasisi husika.

Licha ya kuwa mifumo mingi ya usafi imeundwa kwa kuzingatia vigezo hivyo, mifumo hiyo kwa desturi imegunduliwa haitimizi vigezo hivyo na hivyo huporomoka kila wakati. Kwa uhalisia hakuna mfumo wowote unaotimiza vigezo vyoye vya uhimiliki. Uhimiliki ni dira au uelekeo wala sio hatua ya kuafikiwa. Hata hivyo ni muhimu kwamba mifumo ya usafi ichunguzwe na kuhakikiwa kwa makini kwa kuzingatia nguzo zote za uhimiliki. Kwa vile hakuna suluhu moja inayotimiza nguzo zote za uhimiliki kwa kila tatizo la usafi katika hali mbali mbali na kwa kiwango sawa, uhakiki wa mfumo wowote ule utategemea hali zilizopo na kulazimika kuangazia hali za wakati huo kimazingira, kiteknolojia, kijamii na kitamaduni na kiuchumi. Kwa kuzingatia nguzo zote za uhimiliki, ni muhimu kutilia maanani kanuni za kimsingi katika kuandaa, kusanifu na kutekeleza mfumo wa usafi. Kanuni hizi tayari ziliasisiwa hapo awali na kuidhinishwa Novemba 2000 na wanachama wa baraza la pamoja la ugavi wa maji na usafi katika mkutano wao wa tano. Kanuni hizi ndizo zijulikanazo kama "*Bellagio Principles for Sustainable Sanitation*". Kanuni hizi ni kama ifuatavyo:

(1) Kuzingatiwa kwa dhana za: utu, hadhi na ubora wa maisha na dhamana ya mazingira katika kaya/nyumba.

(2) Kushirikishwa kwa washika dau wote hususan watumizi na watoa huduma za usafi mintarafu ya kanuni za uongozi mwema, na maamuzi.

(3) Uchafu au taka hauna budi kuangaliwa kama rasilimali na usimamizi wake uwe jumlishi na kutangamanishwa na rasilimali za maji, mtiririko wa virutubishi na usimamizi wa mfumo wa uzoaji na usafishaji taka.

(4) Miktadha na viwango vya kusuluhisha matatizo ya usafi vinafaa kuwa katika kiwango cha chini kama vile kiwango cha nyumbani, ujirani, jamii, mji, wilaya na miji mikuu,

## Lengo na madhumuni ya Muungano wa Mashirika tekelezi ya Usafi Himiliki

Lengo kuu la Muungano wa Mashirika tekelezi ya Usafi Himiliki ni kuchangia katika kufanikisha malengo ya milenia kwa kueneza mifumo himiliki ya usafi. Muungano huu unaenzi na kushabikia malengo ya milenia na Mwaka wa Kimataifa wa Usafi kwani hutetea sana hali ya usafi na kuufanya upate kipa-umbele katika ajenda za maendeleo. Kazi ya muungano huu ni kuchangia katika utekelezi wa mifumo himiliki ya usafi kwa kiwango kikubwa, kuandaliwa na kufanikishwa kwa programu za maji na usafi mintarafu ya mikakati iliyopendekezwa na WHO, UNDP-PEP, UNSGAB na UNESCO.












**Malengo ya jumla ya Muungano wa Mashirika tekelezi ya Usafi Himiliki :**

- Kukuza ufahamu na utambuzi wa watu duniani kuhusu mitazamo mbali mbali ya usafi himiliki;
- Kuangazia umuhimu wa usafi himiliki katika kufanikisha malengo yete ya milenia (K.v. kupunguza idadi ya vifo vya watoto wachanga, kukuza usawa wa kijinsia, kuhakikisha uhimiliki wa mazingira, kuimarisha riziki na kupunguza umasikini);
- Kuonyesha jinsi miradi ya usafi inavyofaa kupangwa na kuratibiwa pamwe na ushirika wa washika dau ili kupata maoni ya watumizi.

**Malengo mahususi ya Muungano wa Mashirika tekelezi ya Usafi Himiliki:**

- Kukusanya na kuweka pamoja habari zitakazowasaidia waamuzi (pamoja na umma) kutathmini mifumo tofauti ya usafi na teknolojia kwa kuzingatia vigezo vya uhimiliki;
- Kuonyesha jinsi mifumo ya usafi inayozalisha vikolezo vya uimarishaji wa udongo, mbolea, bayogesi na maji ya unyunyiziaji inavyoweza kuchangia katika kuafikiwa kwa malengo ya milenia;
- Kukusanya na kuwasilisha mifano ya utekelezi bora wa usafi katika mwaka wa Kimataifa wa Usafi na baadaye;
- Kutambulisha na kuelezea utaratibu wa kuimarisha utekelezi wa mifumo himiliki ya usafi pamoja na jinsi ya kuifadhili na utoaji wa huduma za usafi kwa jamii maskini.
- Kutoa mwongozo wa kimataifa wa jinsi mitazamo himiliki huchangia kuafikiwa kwa malengo ya usafi katika ule msururu wa malengo ya milenia na kuunga mkono Mwaka wa Kimataifa wa Usafi na baadaye.

## Namna ya kuafikia malengo yaliyokusudiwa

Utaratibu wa pamoja

Ili kuafikia malengo yaliyoorodheshwa hapo juu, utaratibu wa pamoja wa shughuli zinasohusiana na usafi himiliki kwa minajili ya Mwaka wa Kimataifa wa Usafi ulizinduliwa na washiriki kutoka mashirika zaidi ya 30 na taasisi za utafiti katika mikutano ya Januari na Aprili 2007. Mpango huu wa pamoja unahusisha msururu wa vikundi tendi/tekelezi ambavyo kwa pamoja vitafafanua na kuchanganua makala yaliyochapishwa kuhusiana na usafi himiliki. Pia vikundi hivi vitapanga na kuchangia katika shughuli za kimataifa na kuchangia katika amali za kufadhili na kukuza uwezo na tajiriba ya usafi himiliki.

## Mwaliko wa kujiunga na Muungano wa Mashirika tekelezi va Usafi Himiliki

Muungano wa Mashirika tekelezi ya Usafi Himiliki sio shirika jipya bali ni mtandao wa mashirika yanayojishughulisha na maswala ya usafi himiliki na ni wazi kwa wanaotaka kujiunga nao katika kueneza mifumo ya usafi himiliki. Muungano huu unaalika mashirika mengine ya kitaifa na kimataifa kujiunga nao, kuchangia na kuwa wanachama shiriki/tendi katika vikundi mbalimbali vya muungano huu. Maoni kuhusu namna ya kuuimarisha ule utaratibu wa pamoja unakaribishwa kwani ni utaratibu unaoimarishwa kila uchao na u(na)tahusisha shughuli zote zinazo/zitakazochangia utekelezi zaidi wa mifumo himiliki ya usafi.

## Kwa habari zaidi tafadhali wasiliana na:

info@susana.org
www.susana.org
Roland Schertenleib (EAWAG – SANDEC)
Arne Panesar (GTZ)

*Tafsiri hii imetafsiriwa kwa niaba ya SuSanA na:*
***Raphael Mwaura Gacheiya***
*gacheiya@yahoo.com*
*Afisa mwelekezi wa mradi wa ROSA*
*Nakuru- Kenya*

*Chini ya usimamizi wa:*
***Dr. Benedict M. Mutua***
bmmutua@yahoo.com
Mkuu wa Kitivo cha Uhandisi na Teknolojia - Chuo Kikuu cha Egerton.
(Dean Faculty of Engineering & Technology - EGERTON UNIVERSITY)
*BOX 536- Njoro Kenya*










## Literature

**GTZ (2003):** “10 Recommendations for Action from the Luebeck Symposium on ecological sanitation, April 2003.” http://www.gtz.de/de/dokumente/en-ecosan-recommendations-for-action-2003.pdf

**IWA (2007):** Sanitation21 – simple approaches to complex sanitation. A draft framework for analysis, http://www.iwahq.org/uploads/iwa%20hq/website%20files/task%20forces/sanitation%2021/Sanitation21v2.pdf

**SEI (2005):** “Sustainable pathways to attain the Millennium Development Goals - Assessing the role of water, energy and sanitation” http://www.ecosanres.org/pdf_files/MDGRep/MDG_folder.pdf

**SuSanA website: www.susana.org** – contains publications of working groups, case studies, minutes from SuSanA meetings, etc.

**UNDP HDR (2006):** Human Development Report 2006 - Beyond scarcity: Power, poverty and the global water crisis. http://hdr.undp.org/hdr2006/pdfs/report/HDR06-complete.pdf

**UNDP PEP (2006):** “Poverty Environment Partnership Joint Agency Paper on Poverty Reduction and Water Management” http://www.who.int/entity/water_sanitation_health/resources/povertyreduc2.pdf

**UNESCO-GTZ (2006):** “Capacity building for ecological sanitation.” http://www2.gtz.de/Dokumente/oe44/ecosan/en-ecosan-capacity-building-2006.pdf

**UNSGAB (2006):** The Hashimoto Action plan http://www.unsgab.org/Compendium_of_Actions_en.pdf

**WHO (2006)**: Guidelines series on the safe use of wastewater, excreta and greywater in agriculture and aquaculture. http://www.who.int/water_sanitation_health/wastewater/gsuww/en/index.html

**WSSCC/Sandec (2000):** The Bellagio Statement on Sustainable Sanitation: http://www.eawag.ch/organisation/abteilungen/sandec/publikationen/publications_sesp/downloads_sesp/Report_WS_Bellagio.pdf

### Nembo za mashirika shiriki katika Muungano wa SuSanA kufikia Februari 2009

**Maelezo ya hati miliki**
Vifaa vyote vya SuSanA vinapatikana kwenye leseni wazi ya CC-BY SA. Sahihi kamilifu ya chanzo,sharti ipeanwe wakati vifaa vinatumika.
Kauli ya leseni hii hutumika tu kwenye vifaa vya SuSanA na bali sio kwenye hati/stakabadhi na maonyesho ya wengine ambayo yamepakiwa kwenye maktaba au tovuti ya SuSanA.
Kuhusu zile hati/stakabadhi za wengine, tafadhali tazama vizuri mahala penye leseni zao zinakotoka kabla ya kuzitumia. Katika hali yeyote, kila wakati hakikisha umepeana sahihi ya chanzo.

